

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI**

**03 JUNI, 2026**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI – TAREHE 03 JUNI, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**496. MHESHIMIWA THOMAS KAMPALA MAGANGA (KATAVI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini miundombinu ya Shule ya Mkondo wa Amali Mulele itajengwa ikiwemo nyumba za Walimu na Karakana za Ufundi wa magari na Umeme.

**497. MHESHIMIWA BENJAMIN LUKUBHA NGAYIWA (KAHAMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara za ndani katika Jimbo la Kahama Mjini zitajengwa kwa kiwango cha lami na changarawe ili kuepuka adha ya usafiri.

**498. MHESHIMIWA BARAKA ULIMBOKA MWAMENGO (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka gari la kubebea Wagonjwa katika Kituo cha Afya Ipinda.

**WIZARA YA FEDHA:**

**499. MHESHIMIWA TIMIDA MPOKI FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, hatua gani zimechukuliwa kulinda Biashara na Mitaji ya Vijana dhidi ya ucheleweshaji wa malipo ya madeni ya Wakandarasi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**500. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Mradi wa Umwagiliaji wa Arusha Chini utaanza kujengwa.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**501. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA Wilayani Biharamulo ili kuwawezesha Vijana kujikwamua kutokana na Mafunzo yanayotolewa.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**502. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Minara ya Mawasiliano katika Halmashauri ya Mji Ifakara hasa Ikwambi, Mang'ula B na Kanyenja.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **503. MHESHIMIWA ENG. AMOSY WILLIAM MAGANGA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Maji ya Ziwa Victoria yataanza kusambazwa katika Kata za Pangale, Mpombwe, Igigwa, Kisanga, Tutuo, Mkolye, Chabutwa na Ipoje.

### **504. MHESHIMIWA ESTER AMOS BULAYA (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha zilizobaki za utekelezaji wa Miradi 9 ya Maji yenye thamani ya Bilioni 13 ambapo zimetolewa Bilioni 7 tu.

### **505. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji wa Tsoray utakaohudumia Vijiji 21 katika Halmashuri ya Mji wa Mbulu.

**WIZARA YA UJENZI:**

**506. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO  
(MISSENYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itatenga Bajeti ya kutosha ili kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Katoma - Bukwali badala ya kujenga mita 200 kila mwaka.

**507. MHESHIMIWA SILVERY LUBOJA SALVATORY  
(MISUNGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini upanuzi wa Barabara Kuu kwa njia nne kutoka Kenyatta - Usagara Mwanza utaanza.

**DODOMA  
03 JUNI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD  
KATIBU WA BUNGE**